

Maswali yanayoibuka mara kwa mara kuhusu bima ya Apple Health juu ya ugonjwa wa COVID-19

1. Je, niko kwenye hatari ya kupoteza bima yangu ya Apple Health (Medicaid) wakati wa janga la COVID-19?

Health Care Authority (HCA) na washirika wake watazuia kusimamishwa kwa malipoya huduma ya afya kwa wanufaika wote wa bima ya Apple Health, isipokuwa wakati ambapo mhusika:

- Atawasilisha maombi ya kusitishwa kwa bima yake;
- Si mkazi tena wa jimbo la Washington, au;
- Amefariki

2. Nilipokea barua kwamba bima yangu ya afya ilisimamishwa kutokana na kukosa kujisajili upya. Je, nitafanyaje ili bima yangu ianze kufanya kazi tena?

Ikiwa bima yako ilisimamishwa kutokana na kukosa kujisajili upya, maofisa wanaoshughulikia bima ya HCA watakurudishia bima yako. Utapokea barua ya kuthibitisha hatua hii. Iwapo una maswali au bima yako bado haijarudishwa, piga simu 1-800-562-3022.

3. Je, bado ninapaswa kutoa uthibitisho juu ya ombi langu la kurudishiwa bima iliyosimamishwa?

Iwapo utashindwa kutoa ushahidi wa mapato kutokana na ugonjwa wa COVID-19, HCA itakubali kupokea uthibitisho binafsi wa mapato yako ili kufufua bima yako ya afya kuanzia Februari 2020, na kwa kila mwezi ambapo mapato yako yaliathiriwa na COVID-19.

4. Je, naweza kuomba kuongezewa muda ili niweze kutoa taarifa inayohitajika na HCA au Department of Social and Health Services (DSHS)?

Ndiyo. Tunawapatia wateja wetu siku 30 zaidi ili waweze kutoa taarifa inayohitajika. Unaweza kuwasiliana na HCA kwa namba ya simu 1-800-562-3022, au DSHS kwa namba ya simu 1-877-501-2233.

5. Je, bado unapaswa kutoa taarifa ya mabadiliko?

Ndiyo. Iwapo hupoeki mapato yoyote, ama iwapo ulipoteza mapato kutokana na kuachishwa kazi, unapaswa kutoataarifa ya mabadiliko kwa kufanya maboresho kwenye maombi yaklo.

- 
- 6. Kwa sasa ninanufaika na bima ya Apple Health na sasa mimi ni mja mzito. Je, ninapaswa kutoa taarifa kuhusu uja uzito wangu?**
- Ndiyo. Unapaswa kutoa taarifakuhusu uja uzito wako.
- 7. Tayari ninanufaika na huduma za bima ya Apple Health; je, ninapaswa kutoa taarifa kuhusu mapato yangu ya kutokuwa na ajira, au mafao ya ziada ya \$600 ya kila wiki ya kutokuwa na ajira?**
- Hapana, haina haja ya kutoa taara ya mapato haya iwapo kwa sasa unanufaika na huduma za bima za Apple Health.
- 8. Je, nitaweza kupokea mafao ya ziada ya \$600 ya kila wiki kutokana na hali yangu ya kutokuwa na ajira?**

Ndiyo, watu wengi wasiokuwa na ajira watapokea mafao hayo ya ziada ya kila wiki. Kwa maeleo zaidi, tafadhali somae [Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara yaliyotolewa na WA Employment Security Department](#).

- 9. Je, nitaanza lini kunufaika na ziada ya \$600 ya kila wiki ya kukosa ajira?**
- Jimbo la Washington linatarajia kuanza kutoa mafao haya kuanzia 4/20/2020. Kwa taarifa zaidi, tafadhali somae [Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara yaliyotolewa na WA Employment Security Department](#).
- 10. Nilipokea hundi yangu ya kupunguza Ugumu wa Maisha kutoka Serikali Kuu. Je, ninapaswa kutoa taarifa kuhusu mapato haya?**
- Hapana, usitoe taarifa kuhusu hundi yako ya kupunguza ugumu wa maisha kwa Washington Healthplanfinder. Mapato ya kupunguza ugumu wa maisha hayahesabiwi kwenye bima ya Apple Health.
- 11. Hundi yangu ya kupunguza ugumu wa maisha ni kiasi gidogo kuliko matarajio yangu. Je, nitafanya nini?**

Tembelea tovuti ya [Internal Revenue Service \(IRS\)](#) ili kupata majibu kuhusu hundi yako ya kupunguza ugumu wa maisha.

- 12. Je, bado ninahitajika kulipa malipo ya bima ya Children's Health Insurance Program (CHIP)?**

Iwapo umeathirika na COVID-19, madeni yako ya CHIP yanaweza kufutiliwa mbali iwapo:

- Una uwezo wa kulipia bima ya afya ya CHIP; au
- Umepoteza sifa za CHIP kutokana na kuchelewa kulipa malipo ya bima

13. Ninanufaika na bima ya the Apple Health for Worker's with Disabilities (HWD). Bado ninastahili kunufaika?

Iwapo unaendelea kunufaika chini ya Mpango wa HWD na mapato yako yamepungua, umepoteza ajira ama umesimamishwa kazi kwa muda, unaweza kuendelea kunufaika na bima na malipo yako kusamehewa.

- Piga simu 1-800-871-9275
- Iwapo unaendelea kupokea msaada wa Long Term Services and Supports (LTTS), wasiliana na Afisa wa Mafao ya Umma (Public Benefits Specialist) kwa kutembelea tovuti ya [DSHS Aging and Long-Term Support Administration \(ALTSA\)](#).

14. Mimi si mkazi wa Jimbo la Washington, lakini nilitembelea jimbo hili na sasa mimi ni mgonjwa na nimewekwa katika karantini. Je, naweza kuwasilisha ombi la bima ya Apple Health ili niweze kufanyiwa uchunguzi na kutibiwa?

Iwapo umewekwa karantini katika Jimbo la Washington, unaweza kukubaliwa kwa bima na matibabu ya COVID-19. Tafadhalii piga simu 1-800-562-3022 ili kupata taarifa zaidi.

15. Mimi ninanufaika na bima ya afya kupitia DSHS na kwa kawaida, napaswa kuthibitisha mpato yangu au taarifa za benki. Je, bado nahitajika kutoa taarifa hii kwa kuinakili kwenye karatasi?

Hapana, lakini unaweza kutoa uthibitisho binafsi kuhusu mapato na rasilimali zako wakati unapowasilisha ombi au unapojisajili upya au kutoa taarifa kuhusu mabadiliko. Waweza kuwapigia simu DSHS kwa nambaya simu 1-877-501-2233 ili kuwasilisha taarifa yako.

16. Nilipimwa COVID-19 katika kituo cha kwenye magari na niliwasilisha maombi ya bima ya AEM. Je, ninapaswa kuwasilisha nyaraka gani?

Kila kituo cha uchunguzi wa COVID-19 hutoa hati tofauti. Toa stakabadhi zozote ulizopewa zinazoonyesha umepimwa COVID-19. Pia utapaswa kutoa jedwali na/au hati zozote za matibabu. Hati yoyote uliyopewa na mtoa huduma wako kama uthibitisho itakubaliwa.